AckySHINE.com

# Amri ya Saba ya Mungu: Usiibe - Tambua mali ya mtu na kuheshimu

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · December 19, 2015

Mafundisho ya Katekisimu · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Amri za Mungu

Je, Amri ya Saba ya Mungu inafundisha nini?

Amri ya saba ya Mungu inafundisha kuitambua mali ya mtu na kuiheshimu.

Mali ya mtu ni ipi?

Mali ya mtu ni ile aliyoipata kwa njia halali yaani kwa haki.

Lengo la mali ya binafsi ni lipi?

Kutosheleza mahitaji yake mtu binafsi, ya familia, ya wenye shida na ya kanisa.

Mtu awatendeje wanyama?

Mtu anatakiwa kuwatendea wanyama kwa wema kama viumbe wa Mungu

Amri ya saba ya Mungu inakataza nini?

Inakataza haya;

1. Wizi 2. Kulangua 3. Kutapeli 4. Kughushi 5. Kufuja mali 6. Kutoa au kupokea rushwa 7. Ufisadi 8. Kuharibu mali ya mtu au jamii

Anayejipatia mali kwa njia isiyo ya halali yampasa kufanya nini?

Anayejipatia mali kwa njia isiyo ya halali yampasa kurudisha gharama yake kwa mwenye mali

Anayeharibu mali ya mwingine lazima afanye nini?

Anayeharibu mali ya mwingine lazima alipe hasara aliyosababisha. (Lk 19:8)

Je yatupasa kufanya kazi?

Ndiyo, kwa sababu:

1. Kazi inampa mwanadamu heshima 2. Kufanya kazi ni wajibu wa haki. (Mwa 1:28)

Je ni lazima kuwasaidia masikini na fukara?

Ndiyo, Kuwatendea Masikini mema ni kumtendea Yesu mwenyewe. (Mt 25:40)